**SALAMU ZA MTENDAJI MKUU WA OSHA, BI. KHADIJA MWENDA, KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI, APRILI 28, 2026 - NJOMBE**

**Mheshimiwa Deus Sangu** (MB), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi, Ajira na Mahusiano, Viongozi na wageni wote mliojumuika nasi hapa.

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania….**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**; awali ya yote napenda kumshukuru Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujalia afya njema na kwa neema na baraka zake imempendeza kutukutanisha hapa leo Mkoani Njombe kwenye kilele cha maadhimisho ya siku hii ya Usalama na Afya mahali pa kazi Duniani.

Aidha, nipende kukushukuru **Mhe. Waziri**. kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa Mgeni Rasmi pamoja na majukumu mazito ya kitaifa uliyonayo, hasa katika katika kipindi hiki cha Bunge la bajeti, lakini kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa maadhimisho haya, ulikubali kuwa Mgeni Rasmi kwa kushiriki wewe binafsi katika shughuli hii, kwa niaba ya Menejiment na watumishi wa OSHA nakushukuru sana na karibu sana.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**; Kipekee na kwa heshima kubwa napenda nitumie fursa hii kushukuru wenzetu wa Mkoa wa Njombe chini ya uongozi mahiri wa Comrade Mhe. Antony Mtaka, kwa kukubali kuwa mwenyeji wa maadhimisho haya na hakika wametupatia ushirikiano mkubwa sana wana OSHA hatuna cha kuwalipa zaidi ya kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwapa afya njema tuzidi kuchapa kazi na tujenge Taifa letu.

Halikadhalika, niwashukuru Wadau wetu wa Utatu ambao ni Shirikisho la vyama vya wafanyakazi (TUCTA), Chama cha waajiri Tanzanzia (ATE) na Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kushirikiana nasi katika maandalizi ya maadhimisho haya, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la kazi Duniani (ILO) Kanda ya Afrika Mashariki, **Bi. Caroline Khamati Mugalla,** yeye binafsi pamoja na ofisi yake ambavyo tumekuwa tukishirikiana na kufanyakazi kwa karibu katika kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa mikataba ya kimataifa inayohusu masuala ya usalama na afya. Hakika Shirika la kazi Duniani limekuwa likithamini kazi nzuri inayofanywa hapa nchini katika kusimamia viwango vya kazi, kwa kutambua hilo leo hii, Kiongozi huyu, ameipa heshima Tanzania ya kujumuika nasi leo. Kimsingi Ofisi ya ILO inasimamia kanda ya afrika mashariki yote, **Bi Caroline** angeweza kushiriki katika nchi nyingine ndani ya afrika mashariki lakini ameamua kuungana nasi hakika ni heshima kwa OSHA na kwa Nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla.

**Mheshimiwa Mgeni rasmi**; Niliona ni vyema nikushukuru na kushukuru wadau wetu kwa heshima mliyoulitupatia, kabla ya kukutambusha wageni ambao wamekuja kujumuika nasi katika maadhimisho haya kitaifa mkoani Njombe. Hivyo kwa heshma kubwa , naomba utambue uwepo wageni wafuatao.

- **Mhe. Deo Sanga,** Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe;
- **Mhe. Antony Mtaka**, Mkuu wa Mkoa wa Njombe,
- **Bi. Mary Maganga** Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano

- **Dkt. Stephen Nindi**, Katibu Tawala Mkoa wa Njombe
- **Mhe. Dkt Yose Mlyambina,** Jaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi
- **Bi. Zuhura Yunus,** Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi Ajira na Mahusiano
- **Mhe. Hawa Chakoma Mchafu**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii,
- **Mhe. Dkt. Regina Malima**, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii,
- **Mhe. Lucy Kombani** Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii
- **Mhe. Kangi Lugola** Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii
- **Mhe. Kassim Morgan** Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii
- **Mhe. Juma Sweda**, Mkuu wa Wilaya ya Njombe;
- **Mhe. Zakaria Mwansansu** Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe
- **Wajumbe  wa Kamati ya Usalama Mkoa Njombe,**
- **Ndugu Caroline Khamati Mugalla**, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Kanda ya Afrika Mashariki,
- **Bi. Suzan Mkangwa,** Kamishna wa Kazi
- **Bi. Suzanne Ndomba-Doran**, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE),
- **Ndugu Tumaini Nyamhokya**, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),
- **Ndugu Herry Mkunda**, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya

Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),

- **Dkt .Abdulssalam Omary,** Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)
- **Bw. Fortunatus Magambo** Mkurugenzi Mkuu wa hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)
- **Bw. Masha Mshomba** Mfuko wa Hifadhi ya jamii (NSSF)
- **Mhe. Usekelege Mpulla**, Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi
- **Wafanyakazi wote wa OSHA**
- Viongozi na Wafanyakazi wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi Zake,
- Viongozi wa Dini Mliopo
- Washiriki wa Maonesho wote waliopo,
- Wafanyakazi wote mliopo hapa
- Ndugu Wandishi wa Habari
- Wageni Waalikwa,
- Mabibi na Mabwana.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi:** hawa ni baadhi ya viongozi na washiriki walioweza kufika hapa kushirikiana nasi katika maadhimisho haya siku ya leo. Kwa niaba ya Menejmenti na Watumishi wa OSHA Ninawashukuru na ninawakaribisha sana katika tukio hili muhimu la uhamasishaji wa uwepo wa mazingira salama kwa wafanyakazi mahali pa kazi, kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

**Mheshimwa Mgeni Rasmi:** Waswahili husema, Shughuli ni watu... nami nakubaliana na msemo huo, na kwa heshima kubwa naomba utambue uwepo wa wadau wetu ambao wametuunga mkono katika kufanikisha

shughuli hii, kwa hakika wadau hawa na wengineo wamekuwa nasi siku zote katika kuhakikisha tunafanikiwa kwa pamoja kama Taifa, na hii ni kwa kutambua kuwa maadhimisho haya siku ya leo yanaadhimishwa Dunia nzima . **Mhe. Mgeni Rasmi**, na hapa tunapojivunia kuwa maadhimisho haya yamefana kama ulivyojionea, ni pamoja na michango ya hali ,mali na mawazo ya Wadau wafuatao:

MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA 2026YANALETWA KWENU KWA HISANI KUBWA YA:

- NORTH MARA GOLD MINE LIMITED
- GEITA GOLD MINING LIMITED
- VODACOM TANZANIA PUBLIC LIMITED COMPANY
- TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LTD
- CRDB BANK PUBLIC LIMITED COMPANY –
- NMB BANK PUBLIC LIMITED COMPANY
- GAS COMPANY ( T) LIMITED
- SHANTA MINING COMPANY LIMITED NEW LUIKA GOLD MINE.
- WORKERS COMPENSATION FUND – WCF
- THE NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND(NSSF)
- SBC TANZANIA LIMITED
- HUAWEI TECHNOLOGIES (TANZANIA) COMPANY
- SHAFA AGRO LIMITED Shafa Mills
- ETG INPUTS LIMITED
- TANZANIA COMMERCIAL BANK PUBLIC LIMITED COMPANY
- PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND– PSSSF
- MUFINDI PAPER MILLS LTD.
- DP WORLD DAR ES SALAAM LIMITED
- HONORA TANZANIA PUBLIC LIMITED COMPANY
- AZANIA BANK LIMITED
- MKWAWA LEAF TOBACCO LIMITED –
- TANZANIA SHIPPING COMPANY LIMITED (TASHICO) -–
- TANZANIA CIGARETTE PUBLIC LIMITED COMPANY
- AECI MINING TANZANIA LIMITED
- AKSHAR MINING SERVICES LIMITED

- PUMA ENERGY TANZANIA LIMITED
- BULYANHULU GOLD MINE LIMITED
- KNAUF GYPSUM TANZANIA LIMITED
- SAO HILL INDUSTRIES LIMITED - SAW MILL
- MSA LABORATORIES (T) LIMITED
- MEDICAL STORES DEPARTMENT.
- FIRE AND RESCUE FORCE
- LUSH CHANZO WOOD INDUSTRIES LIMITED
- DUMASPEED COMPANY LIMITED
- TANZANIA BREWERIES PUBLIC LIMITED COMPANY
- AFRICAN ASSAY LABORATORIES (T) LTD
- SAID SALIM BAKHRESA & COMPANY LIMITED
- THE TANZANIA COFFEE RESEARCH INSTITUTE LIMITED - TACRI
- THE NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
- SAS LOGISTICS LIMITED
- SHELYS PHARMACEUTICALS LIMITED
- PLANET PHARMACEUTICAL LTD

Aidha pamoja na Michango hio kutoka kwa wadau, baadhi ya wadau wetu wamechangia pia vifaa ambavyo ni;

MAHITAJI AMBAYO WADAU WAMETUCHANGIA

| S/N | TAASISI | MAHITAJI |
|---|---|---|
| 1. | BARRICK NORTH TANZANIA | Mitungi ya gesi 60, Wanafunzi, Kofia za Usalama , reflectors na kofia Ngumu (40), miwani 25 kwa Bodaboda(25), madaftari (300), na Kufunga Umeme Shule ya Msingi Mji Mwema,Taulo za Kike 100. Vizimia moto Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Njombe (fire extinguisher ) na shuleni mitungi 2. Mitungi ya gesi ya thaman ya Tsh. 22,000,000 |
| 2. | CRDB BANK PLS | Wametoa dawa zenye thamani ya Tsh 33,000,000 na kufanikisha Mafunzo kwa wajasirilimali wakina |

| | | |
|---|---|---|
| | | mama wa Mkoa wa Njombe wakiwemo mama Lishe. |
| 3. | Chuo cha Usafirishaji (NIT) | Wametoa mafunzo kwa maafisa usafirishaji wa mkoa wa Njombe (Boda boda wapatao 200). |
| 4. | NMB | Wametoa Reflector zenye thamani Tsh 15,000,000 kwa maafisa usafirishaji wa Mkoa wa Njombe. |
| 5. | Planet Phamarcy | Dawa kwa ajili ya wananchi wa Njombe thamani Tsh. 55,000,000/ |
| 6. | MSD | Wametoa madawa mbalmbali yenye thamani Tsh. 20,000,000/ |
| 7 | Geita Gold Mine | Wametoa Vifaa Kinga kwa maafisa Usafirishaji vyenye thaman Tsh. 13,000,000/ |

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi:** kwa niaba ya Kamati ya Maandalizi napenda nitumie fursa kutambua michango yenu na ushiriki wenu, katika kufanikisha maadhimisho haya, na Niombe tuendelee kushirikiana katika kuhamasisha na kuimarisha mifumo ya usalama na afya Mahali pa kazi, ili kujenga uchumi wa nchi na kulinda nguvu kazi ya Taifa.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;** Pamoja na kupewa nafasi hii ya kukutambusha baadhi ya wageni tuliounga nao siku ya leo naomba kwa ruksa yako nitumie fursa hii kueleza kwa ufupi dhana na uhalisia wa maadhimisho haya.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;** Tanzania leo inaungana na Mataifa mengine Duniani kuadhimisha siku ya usalama na afya mahali pa kazi. Maadhimisho haya ambayo hufanyika kila mwaka, huandaliwa na Serikali kupitia Taasisi ya OSHA kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni Shirikisho la Vyama

vya Wafanyakazi (TUCTA), Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) pamoja na Shirika la Kazi Duniani (ILO) Pamoja na Mkoa Mwenyeji. Maadhimisho ya mwaka huu mkoani Njombe yanatupatia fursa ya kipekee ya kutimiza miaka 23 tangu kuanzishwa kwake hapa Nchini.

**Mhe. Mgeni Rasmi na Wageni Waalikwa**, sote tunafahamu kwamba Dunia imekuwa ikipitia nyakati mbalimbali katika mapinduzi ya kujenga uchumi wa dunia. Mojawapo ni mapinduzi ya kujenga uchumi kupitia viwanda. Mpaka sasa Dunia imepitia awamu mbili na sasa tupo katika awamu ya tatu na Nne inayohusisha Mapinduzi ya kidigitali, kompyuta, na otomatiki (automation).
Matumizi ya teknolojia ya hali ya juu kama Akili Bandia (AI), Mtandao wa Vitu (IoT), na teknolojia ya kidigitali.

**Mhe. Mgeni Rasmi ;** Katika jitihada hizo za kujikomboa kiuchumi wazalishaji walijikuta, wamejikita zaidi katika kuhakikisha kwamba uzalishajimali unaongezeka ,faida inapatikana ,na uchumi wa makampuni unakuwa, huku athari za kijamii, kiuchumi, mazingira na masuala ya usalama na afya kwa wafanyakazi vikiwa sio kipaumbele, kukosena kwa vipaumbele hivyo kwa wafanyakazi kulipelekea ajali nyingi, kuibuka kwa magonjwa kazi, vifo vilivyotokana na ajali ama mgonjwa na ulemavu na mgonjwa ya kudumu kwa wafanyakazi.

Hii ilipelekea, wafanyakazi kuanza harakati za kudai haki zao ikiwemo suala la usalama na afya mahali pa kazi.

**Mhe. Mgeni Rasmi;** Katika harakati hizo Mnamo**,**tarehe 28 Aprili 1996 katika Jiji la New York, nchini Marekani siku kama ya leo, Kwa mara ya kwanza yalifanyika maandamano makubwa, ikiwa ni jitihada za wafanyakazi

duniani kote kupaza sauti wakidai mazingira salama ya kazi ili kulinda afya na usalama wao wakiwa wanatekeleza majukumu yao ya kila siku.

**Mhe. Mgeni Rasmi;** Lengo la maandamano hayo ilikuwa ni kuwakumbuka wafanyakazi wenzao walioumia wakiwa kazini, waliopata magonjwa yatokanayo na kazi, waliopata ulemavu, pamoja na waliopoteza maisha wakiwa kazini, Tukio hili ilikuwa ni katika kuonesha masikitiko, maumivu na mshikamano wakudai haki huku waandamanaji wakiweka mashada ya maua na kuwasha mishumaa kama ishara ya heshima kwa wenzao, wakitumia fursa hiyo kuwasilisha ujumbe kwa waajiri na jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kuwepo kwa mazingira salama mahali pa kazi.

**Mhe. Mgeni Rasmi**: hapo awali, maadhimisho haya yalikuwa yakiratibiwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Duniani chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo Endelevu la Umoja wa Mataifa. Ilipofika Mwaka 2001, Shirika la Kazi Duniani (ILO) liliunga mkono juhudi hizo za Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi katika kuadhimisha siku hii, na baadae mwaka 2003 ILO ilishawishi kubadilisha maudhui ya maadhimisho haya kwa kupendekeza kuwa siku hii mbali na kuwakumbuka waathirika wa ajali na magonjwa kazini, siku hii ilielekezwa kuwa jukwaa la kuhamasisha uboreshaji wa mazingira ya kazi kwa lengo la kuzuia ajali, magonjwa, vifo, pamoja na kulinda rasilimali za uzalishaji.

**Mhe. Mgeni Rasmi,** kwa heshima ya wafanyakazi wote Duniani, waliopata ajali, waliopoteza maisha, waliopata ulemavu na magonjwa ya kudumu kutokana na kazi naomba ikupendeze tusimame kwa dakika moja... kuwakumbuka wenzetu na kuthamini mchango katika maendeleo ya Dunia.

**Mhe. Mgeni Rasmi;** Nchi yetu ni Mwanachama wa Shirika la Kazi Duniani hivyo imeendelea kukishiriki kikamilifu katika maadhimisho haya kwa kushirikiana na Chama cha waajiri Tanzania (ATE), Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (TUCTA) na Shirika la kazi Duniani (ILO) wa lengo la kulinda haki, utu na ustawi wa wafanyakazi kama msingi wa maendeleo ya taifa.

**Mhe. Mgeni Rasmi,** Kila mwaka maadhimisho haya huambatana na ujumbe mahususi. Kwa mwaka huu, kauli mbiu kutoka Shirika la Kazi Duniani (ILO) inasisitiza kuwa: **"Mazingira Bora ya Kazi Kisaikolojia ni Njia ya Kuimarisha Ustawi wa Wafanyakazi na Kujenga Taasisi Imara"** *(Good Psychosocial Working Environment: A Pathway to Thriving Workers and Strong Organisation).* Kauli mbiu hii inatukumbusha juu ya umuhimu wa kuboresha mazingira ya kazi katika namna ambayo yataleta ustawi wa wafanyakazi kimwili na kiakili. Mazingira bora ya kazi kisaikolojia hutokana na juhudi za makusudi za waajiri katika kutambua, kudhibiti na kupunguza vihatarishi vya kisaikolojia mahali pa kazi.

**Mhe. Mgeni Rasmi; Wageni Waalikwa; Mabibi na Mabwana,** Kimataifa, masuala ya vihatarishi vya kisaikolojia mahali pa kazi yamepewa kipaumbele kikubwa na taasisi mbalimbali za kimataifa zikiwemo International Labour Organization na World Health Organization. Taasisi hizi zinaeleza wazi kuwa vihatarishi vya kisaikolojia ni sehemu muhimu ya afya na usalama kazini, na vinatokana na namna kazi zinavyobuniwa, kusimamiwa pamoja na mazingira ya kijamii ya kazi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;** Hali hii pia inaonekana hapa nchini Tanzania, ambapo mabadiliko ya haraka ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia yameongeza changamoto hizi. Ukuaji wa viwanda, upanuzi wa sekta ya huduma pamoja na matumizi ya teknolojia za kidijitali umeongeza matarajio na mzigo wa kazi kwa wafanyakazi.

Ingawa mfumo wa usalama na afya kazini nchini umefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kudhibiti vihatarishi vya kimwili, bado eneo la vihatarishi vya kisaikolojia halijapewa uzito unaostahili. Hali hii imesababisha maeneo mengi ya kazi kukosa mifumo madhubuti ya kutambua, kuripoti na kudhibiti msongo wa mawazo na changamoto nyingine za kisaikolojia.

**Mhe. Mgeni Rasmi**; Tangu tulipoanza kuadhimisha siku hii mnamo mwaka 2004, kumekuwa na maendeleo chanya katika kuimarisha uelewa na utekelezaji wa masuala ya usalama na afya kazini. Mafanikio haya yanaonekana kupitia ongezeko la ushiriki wa wadau katika maadhimisho, kuongezeka kwa maeneo ya kazi yanayosajiliwa na kukaguliwa, pamoja na ongezeko la wafanyakazi wanaopatiwa huduma za uchunguzi wa afya na mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mgeni rasmi Katika Kipindi cha kuelekea Maadhimisho ya siku ya usalama na afya duniani, OSHA iliendesha kampeni maalum ya Mafunzo

ya kuwajengewa Ulewa kwa wadau na Wajasiriamali wapatao 5677 kati ya 4500 ambao tuliweka lengo la kuwafikia, Wadau hao pamoja na kupatiwa mafunzo pia walipewa Vitendea Kazi (PPE) ambazo ni Kofia Ngumu Reflectors,gloves, Miwani na Vifaa hivi walipewa kulinga na kazi wanazozifanya. Thamani ya vifaa kinga tajwa ni Tsh. 124,000,000/= ambazo Serikali imegharamia. Kwa uchache tu wadau na wajasiriamali walionufaika kwenye Mafunzo haya yalifanyika kwa Kipindi cha Januari hadi Aprili ni wafuatao:

- Wanawake Wachimbaji wa Dhahabu Bukombe (WAWABU)
- Akinamama watengenezaji Batiki na Sabuni Ilala
- Tume ya Utumishi wa Mahakama
- Maafisa waandamizi wa Jeshi la Magereza
- Wafanyakazi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete
- Shirika la Lisilo la Kiserikali linalojihusisha na kuwajengea uwezo jamii za wafugaji PINGOS Arusha
- Taasisi Foresta inajihusisha na kuwawezesha wakulima Vijijini kufanya kilimo cha kisasa kwa kutumia mbole zisizo na Kemikali
- Wakina mama wabanguaji Korosho Mtwara kupitia kikundi cha wakinamama cha Laki Moja
- Maafisa Uhamiaji
- Ofisi ya Rais Menejment ya Utumishi wa Umma
- Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu
- Wafanyakazi wa Halmshauri za Mkoa wa Njombe
- Wananachama wa ATE
- Mafundi mbalimbali hapa Njombe kupitia Fundi Smart
- Akinamama Wafanyabiashara na mama lishe wa Mkoa wa Njombe
- Maafisa Usafirishaji wa Mkoa wa Njombe.

Katika kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050 hususani nguzo ya pili inayosisitiza juu ya kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani pamoja na nguzo ya pili inayozungumzia kujenga uwezo wa watu na maendeleo ya jamii. Nguzo hizo zinasisitiza

Mhe. Mgeni rasmi aidha nipende kusema kuwa OSHA inatekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050 hususani nguzo ya pili, inayolenga kujenga jamii yenye afya, nguvu kazi yenye ujuzi na uchumi shindani, hivyo OSHA ina jukumu la msingi katika kuhakikisha mazingira ya kazi yanakuwa salama. Pia kwenye malengo na shabaha dira imesisitiza ajira zenye staha, kuongeza umri wa kuishi na afya njema inayolinda utu wa mfanyakazi.

Kwa muktadha huo, MAmlaka itaendelea kuimarisha ukaguzi wa mifumo ya usalama na afya kazini katika sekta zote ikiwemo sekta isiyo rasmi, kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za ajali na magonjwa yatokanayo na kazi., pamoja na kuongeza elimu na uhamasishaji kwa wadau kuhusu haki na wajibu wao. Vilevile OSHA itaendelea kushirkiana na sekta mbalimbali katika kuboresha sera na kanuni za usalama na afya ili ziendane na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya dunia ya ulimwengu wa kazi, kwa lengo la kuhakikisha ajira zenye staha, kulinda afya na ustawi wa wafanyakazi na hivyo kuchangia kikamilifu katika utekelezaji wa Dira ya 2050 ya maendeleo endelevu ya Taifa.

OSHA inalitambua mchango na umuhimu wa sekta isiyo rasmi kiuchumi( Informal Economy) na hivyo tutaendelea kuhakikisha Kundi hili linafanya kazi katika mazingira salama na yenye afya kwa kuendelea kutoa elimu, vifaa kwa kushirikiana na wadau wengine ili kufanikisha ukuaji wa kiuchumi na maendeleo jumuishi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;** katika kutekeleza hayo yote kwa mwaka huu OSHA tumejipanga kutekeleza shughuli mbali mbali zinazolenga kuhamasisha utekelezaji wa **Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, Sura Namba 297, Toleo la mwaka 2023** kupitia matukio yafuatayo:

- Kufanya mafunzo mbalimbali ya Usalama na Afya kazini kwa makundi mbali mbali ya wajasiriamali wadogo wanaofanya shughuli mbalimbali zikiwemo kilimo, uchimbaji madini, biashara ndogo ndogo, viwanda vidogo na sekta ya misitu.

- Kuandaa maonesho/ matamasha yanayolenga kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa Sheria na taratibu mbalimbali za usalama na afya katika sehemu za kazi.
- Kutoa tuzo kwa waajiri wanaozingatia vyema viwango vya usalama na afya, ambao watatangazwa na kukabidhiwa zawadi katika hafla maalum itakayofanyika usiku wa Aprili 29, 2026.
- Bonanza la Michezo miongoni wa waajiri na wafanyakazi kwa lengo la kuendelea kutoa hamasa juu ya uzingatiaji wa kanuni bora za usalama na afya kazini pamoja kujenga umoja na mshikamano miongoni mwa wadau wetu wote wa masuala ya Usalama na Afya mahali pa kazi.
- Kuandaa na kuendesha kliniki Maalum ya uchunguzi wa magonjwa yatokanayo na kazi, magonjwa yasiyoambukiza, magonjwa ya kawaida ikiwemo kansa na magonjwa ya akinamama.

Katika maadhimisho ya siku ya usalama na afya mwaka huu, takribani maeneo ya kazi 120 yameshiriki katika maonesho pamoja na wajasiriamali wadogo wapatao 70 ambapo kumekuwa na mwitikio mkubwa ukilinganisha na mwaka jana ambapo maeneo ya kazi yapatayo 90 tu ndiyo yaliyoshiriki ikiwemo wajasiriamali 15. Aidha, kwa mwaka huu washiriki 220, wameshiriki

katika shindano la tuzo ukilinganisha na washiriki 80 wa mwaka jana.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**; Kupitia programu hii jumla ya wajasiriamali wadogo **6,101** walipewa mafunzo katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Geita, Arusha, Lindi, na Dar es Salaam. Idadi hiyo inafanya wajasiriamali waliofikiwa na kupatiwa mafunzo kupitia programu ya Afya Yangu-Mtaji Wangu kufikia 15,101 tangu programu hii ilipoanzishwa mwaka 2024.

Vilevile, OSHA imetoa mafunzo kwa Maafisa Biashara wa mikoa na wilaya zote za Kanda ya Kaskazini nchini wapatao 50.
Mafunzo kwa Maafisa Usafirishaji wapatao 300 Mkoani Njombe ambao walipatiwa refelective Jacket.saduku la huduma ya kwanza pamoja na kofia ngumu, mafunzo haya yalikuwa na ujumbe wa uendeshaji salamu ni nguzo kwa wafilia yangu.
Mafunzo kwa mafundi wapatao 1000, waitwao fundi smart ambao nao walipatiwa vifaa kinga vya aina mbali mbali kutokana na kazi zao na viatarishi vinavyowakabili.
**Mafunzo hayo yote kwa makundi tajwa yamegharamiwa na Serekali kupitia wakala wa usalama na afya ( OSHA).**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**; Kwa kuhitimisha ningependa kuwakumbusha waajiri, wafanyakazi na umma kwa ujumla kuendelea kutekeleza wajibu wao kuhusiana na uimarishaji wa mifumo ya usalama na afya katika maeneo yao ya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Usalama na Afya Mahala pa kazi ikiwemo kuhakikisha kwamba maeneo yao ya kazi yamesajiliwa na OSHA ili wataalam wetu waweze kuwafikia kwa ajili ya ukaguzi wa mifumo

iliyosimikwa na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusiana na usalama na afya kazini.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, mwisho japo si kwa umuhimu, naomba nikushukuru tena wewe binafsi na viongozi wote ulio ambatana nao. Aidha, shukrani hizi ziwaendee wadau wetu wote pamoja na wananchi wa Mkoa wa Njombe na mikoa jirani ambao wameweza kuungana nasi leo katika maadhimisho haya.

Kwa niaba ya watumishi wenzangu wa OSHA, wadau wetu wa utatu ATE, TUCTA na ILO, tunawakaribisha na kuwawatakia maadhimisho mema.

**Asanteni sana.........,**

,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,